**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**612** **URAIA**

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2019**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu Maswali **yote** katika sehemu **A** na mawasali mawili katika kila sehemu **B** na **C**
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na kila sehemu **B** na **C** zina alama **thelathini (30).**
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhiswa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (ALAMA 40)

Jibu maswali **yote**

1. Onesha kwa hoja nne namna gani raia wanaweza kushiriki katika Serikali za Mitaa.
2. Bainisha vipengele vinne vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania vyenye uhusiano na mada mbalimbali za somo la Uraia.
3. Onesha umuhimu wa uhuru wa Mahakama kwa kutoa hoja nne.
4. Taja mambo manne ya kuzingatia katika kutumia kitabu cha kiada.
5. Orodhesha athari nne za kutokuwa macho na utamaduni wa kigeni nchini Tanzania.
6. (a) Toa maana ya zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia,
   (b) Taja aina tatu za zana za kufundishia na kujifunzia kwa kutoa mifano.
7. Bainisha viashiria vya utandawazi kwa kutumia hoja nne.
8. Taja sifa nne za malengo mahsusi katika Muhtasari wa somo la Uraia.
9. Kwa kutumia hoja nne, kuonesha umuhimu wa nukuu za somo kwa mwalimu wa somo la Uraia.
10. Taja manufaa ya maswali ya kuchagua katika somo la Uraia kwa kutumia hoja nne.

## SEHEMU B (ALAMA 30)

Jibu maswali **mawili (02)**

11. Fafanua kwa kutumia hoja tano umuhimu wa ushindani wa kidemokrasia katika siasa ya vyama vingi nchini Tanzania.
12. Chambua athari tano za ukiukwaji wa haki za watoto ndani ya familia.
13. Kwa kutumia hoja sita, kueleza namna Tanzania inavyonufaika na uchumi wa soko huria.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU C (ALAMA 30)

Jibu maswali **mawili (02)**

14. Eleza mambo matano ya kuzingatia wakati wa kufundisha stadi katika somo la Uraia.
15. Chambua mambo sita muhimu ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana za kufundishia.
16. Fafanua misingi sita ya kufuata wakati wa kufanya tathmini katika somo la Uraia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org